*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 158-172*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Utoaji Majina ya Mifugo katika Gɪrɪ̣mi: Uchunguzi wa Gɪ̣irwana

*Rehema Stephano*[1]

## Ikisiri

Makala hii inahusu uchunguzi wa utoaji wa majina ya mifugo katika lugha ya Gɪrɪ̣mi, hususani katika lahaja ya Gɪ̣irwana. Lengo kuu la makala hii ni kubainisha majina pamoja na vigezo vinavyotumika kutoa majina kwa mifugo katika jamii ya Gɪrɪ̣mi. Utafiti uliozaa makala hii umetumia mbinu ya usaili katika kukusanya data, ambapo wafugaji kumi (10) wa jamii ya Gɪ̣irwana kutoka kijiji cha Mpoku kilichopo wilaya ya Singida (Vijijini) walisailiwa. Matokeo yameonesha kuwa vigezo vikuu vinavyotumika katika utoaji wa majina ya mifugo katika Gɪrɪ̣mi ni vinne ambavyo ni umri, ujinsi, rangi na dosari. Ng'ombe huitwa kwa kutumia ujinsi na rangi, dosari (ulemavu), na umri na ujinsi. Mifugo mingine kama mbuzi, kondoo na kuku hutumia umri na ujinsi isipokuwa punda ambaye anatumia kigezo kimoja tu cha umri kwa sababu punda walio wengi wana rangi ya hudhurungi na wachache sana wana rangi nyeupe, na, aghalabu, matumizi makubwa ya punda ni kufanya kazi bila kujali jinsi. Aidha, matokeo ya utafiti yameonesha kuwa katika hatua ya kuzaliwa, mifugo mingi huwa na majina yanayofanana. Majina huanza kugawanywa kwa kuzingatia ujinsi katika hatua ya pili. Makala hii inapendekeza uchunguzi zaidi wa utoaji wa majina ya mifugo kuendelea kufanyika ili kuimarisha mawasiliano katika jamii mbalimbali za wafugaji na kuyahifadhi majina hayo kwa ajili ya vizazi vijavyo.

## 1.0 Utangulizi

Utoaji wa majina kwa vitu mbalimbali ni zoezi la lazima katika jamii kwa lengo la kutofautisha kitu kimoja na kingine. Okal (2012:27), akisisitiza umuhimu wa majina, anasema:

> Kila kiumbe na hali hupewa majina ili kurahisisha mawasiliano na kusaidia katika utambuzi wa haraka wa kinachozungumzwa. Neno linalotumika kutaja viumbe au hali hujulikana kama nomino. Nomino huwapa watu na vitu utambulisho na ni muhimu katika mawasiliano baina ya watu. Nomino ni muhimu katika utambuzi wa kinachorejelewa na kuashiriwa.

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Kiswahili, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Tanzania. Baruapepe: rest_tz@yahoo.com

Kimsingi, nomino (majina) ni mojawapo ya aina za maneno yanayounda lugha. Dhima kuu ya lugha yoyote ile ni mawasiliano. Ingawa kila neno katika lugha yoyote lina thamani yake katika kukamilisha dhima ya mawasiliano katika lugha, Montagnes (1991) anasema kuwa aina za maneno hutofautiana kiuzito katika kuunda sentensi madhubuti. Yeye anapanga aina za maneno kiuzito kuanzia aina ya kwanza hadi ya mwisho kwa mfuatano wa kitenzi, nomino, kiwakilishi, kielezi, kihusishi, kiunganishi na kibainishi. Kwa hali hii, tunaona kwamba nomino inachukua nafasi ya pili ya uzito. Kwa hiyo, ina nguvu na uzito mkubwa katika kuunda sentensi ambayo ndio msingi wa mawasiliano. Kutokana na umuhimu huu wa nomino katika kuwezesha mawasiliano, utafiti huu umefanyika ili kuona jinsi jamii ya Gịirwana inavyowasiliana kupitia utoaji wa majina kwa mifugo yake.

Gịrịmi ni lugha inayozungumzwa katika mkoa wa Singida uliopo Kanda ya Kati nchini Tanzania. Mzungumzaji wa lugha huitwa Mụrịmi (wingi wake ikiwa ni Arịmi). Kwa Kiswahili, neno hili linamaanisha mkulima. Kundi la lugha hii ni F32. Jina maarufu la lugha hii ni Gịnyatụrụ (kwa matamshi ya Kiswahili ni Kinyaturu). Kwa hiyo, wazungumzaji wa lugha hii huitwa Anyatụrụ (Wanyaturu) pia. Gịnyatụrụ ni lakabu ambayo ilitolewa na Wanyamwezi ambao ni majirani kwa upande wa Magharibi wa Arịmi. Arịmi wanawaita Wanyamwezi *Anyamweri* (wa Magharibi). Inasemekana kuwa, Arịmi walipokuwa wakiwinda, walifuatilia miguu ya wanyama na kusema *mụghụụ tụrụ* (mguu huu). Kutokana na neno *tụrụ*, Wanyamwezi wakawaita Anyatụrụ, yaani 'wenye huu' (Mdachi, 1991). Hata hivyo, jina la lugha hii linalotambulika sana katika maandishi ni Gịrịmi (Stephano, 2019). Gịrịmi imegawanyika katika makundi lahaja tatu: Gịirwana, Gịahi (Chahi) na Gịnyamụnying'anyi (Stephano, 2019). Hamasa ya kuchunguza utoaji wa majina ya mifugo katika Gịirwana imesababishwa na kudokezwa kwa majina ya ng'ombe dume na Olson (1964) katika Gịirwana. Yeye aliyataja bila kufafanua kwa undani mofolojia na semantiki yake. Vilevile, Olson (1964) alijadili majina ya ng'ombe tu bila kujiingiza katika mifugo mingine. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza utoaji wa majina ya mifugo kwa jamii ya Gịirwana kwa kuhusianisha na mofolojia na semantiki ya majina hayo.

## 2.0 Maandiko kuhusu Isimu ya Gịrịmi

Lugha ya Gịrịmi haijaandikiwa sana. Hata hivyo, yapo maandiko machache yanayohusu isimu ya Gịrịmi. Mathalani, kuna andiko la Olson (1964) kuhusu fonolojia na mofolojia ya Gịrịmi. Katika utafiti wake, amechunguza zaidi vipengele vya fonolojia kama sauti na mofolojia kwa ujumla. Hata hivyo, licha ya uchunguzi wake kuegemea katika jamii ya Gịrịmi, Olson hajachunguza mofolojia na semantiki ya utoaji wa majina ya mifugo ijapokuwa amegusia majina ya ng'ombe dume katika kujadili ngeli ya kwanza ya nomino ya Gịrịmi.

Wilson (2014) alifanya utafiti kuhusu tofauti za kimsamiati katika lahaja za Kinyaturu. Katika utafiti wake, alichunguza tofauti za msamiati wa aina nyingine

bila kuangalia utoaji wa majina ya mifugo. Stephano (2019) aliandika kuhusu uradidi na mbadala wake kwa kujikita katika Gịirwana. Naye hakugusia kabisa masuala ya utoaji wa majina ya mifugo katika lugha hiyo. Pamoja na maandiko haya matatu, Olson (1964) anatambulisha maandiko mengine mawili aliyopata kuyajua kabla ya kuandika kazi yake. Nayo ni *Abriss einer Grammatic der Kinyaturu Sprache* ya Schregel (1913) na *Une Grammaire Rimi* la Verhoeven ambalo halikuchapishwa. Olson, ijapokuwa hajasema wazi ni vipengele gani vya kiisimu vilijadiliwa katika maandiko hayo, anasema maandiko haya mawili hayakugusia irabu saba za Gịrịmi. Kutogusiwa kwa suala la utoaji wa majina ya mifugo katika tafiti zilizotangulia katika Gịrịmi kumetoa mwanya wa kukitafiti kipengele hicho na kujua vigezo vinavyotumika kutoa majina kwa mifugo mbalimbali ambavyo ni ujinsi, rangi, umri na dosari kwa kuhusianisha na mofolojia na semantiki ya majina hayo.

**3.0 Maandiko kuhusu Utoaji wa Majina ya Wanyama na Ndege**

Majina ni utambulisho wa vitu vinavyoonekana na visivyoonekana. Majina hutambulisha viumbe hai na visivyo hai. Kila kitu kina jina lake. Kwa hiyo, majina yoyote yale, yawe ya watu au vitu, huwezesha mawasiliano kwa sababu ni kirejeleo cha kinachowasilishwa katika mazungumzo na maandishi. Kutokana na umuhimu wa majina katika jamii, watafiti wengi wametafiti na kuandika kuhusu utoaji wa majina kwa vitu mbalimbali, wanyama wakiwamo.

Olson (1964) anabainisha majina ya ng’ombe dume katika Gịrịmi. Anasema kuwa majina ya ng’ombe dume yapo katika ngeli ya (*Ø*-) na *2a* (*vaa*-) na yanatokana na majina ya ng’ombe jike ambayo huambikwa viambishi awali *gí*- na *gídǻ*-, yaani maumbo ambayo huwekwa kabla ya majina ya ng’ombe *jike*. Kwa hiyo, mofolojia inayotambulisha ng’ombe dume ni *gí* na *gídǻ*. Olson anaorodhesha majina ya ng’ombe dume kama vile *gídǻmaa* (mweusi mwenye kichwa cheupe), *gídǻmpondo* (wa kijivu iliyoiva), *gínyiisi* (wa kijivu nyeupe), *gísamu* (wa chuichui), *gíbuuda* (ana korodani moja), *gínawiida* (hana korodani tangu kuzaliwa), na *gítumpi* (ana mkia mfupi), kwa kutaja mifano michache.

Ingawa Olson anasema majina ya ng’ombe dume yanatokana na majina ya ng’ombe jike, anatoa mifano ya majina ya ng’ombe dume tu pasi na kuwasilisha majina ya ng’ombe jike. Kwa hiyo, bado hoja anayotoa kuhusu utoaji wa majina ya ng’ombe dume kutokana na majina ya ng’ombe jike haiko bayana. Makala hii imewasilisha majina ya ng’ombe jike sambamba na majina ya ng’ombe dume ili kuonesha mabadiliko yanayoweza kujitokeza baada ya uambikaji wa viambishi vinavyosimamia majina ya ng’ombe dume. Vilevile, Olson amejikita katika majina ya ng’ombe tu na kuacha majina ya mifugo mingine kama vile mbuzi, kondoo, punda na kuku. Utafiti huu umechunguza utoaji wa majina ya ng’ombe pamoja na mifugo mingine. Aidha, Olson amechanganya vigezo vya uainishaji wa ng’ombe vya ujinsi na ulemavu. Mathalani, *gítumpi* (ng’ombe mwenye mkia mfupi) anaweza kuwa jike pia. Hata hivyo, utafiti wa Olson ni wa muhimu katika uandishi wa makala hii kwa sababu unaweka msingi wa kuchunguza utoaji wa majina ya mifugo katika Gịrịmi, hasa Gịirwana.

Ohta (1987) alitafiti kuhusu utambuzi na utoaji wa majina kwa wanyama katika jamii ya Turkana iliyopo Kaskazini Mashariki mwa Kenya. Alionesha kuwa kigezo kikubwa kabisa cha kutoa majina kwa wanyama ni umri na ujinsi. Vigezo vingine ni rangi ya ngozi, umbo la pembe na umbo la sikio. Hii ina maana kuwa ng'ombe huweza kupewa jina kutokana na mwonekano wa pembe, sikio au kwa kuangalia umri na jinsi yake.

Kuhusu umri na ujinsi, Ohta (1987) anasema kwamba kuna hatua kubwa tatu za ukuaji wa wanyama ambazo huambatana na utoaji wa majina. Katika hatua ya kwanza, dume na jike wanakuwa na majina yanayofanana hata kama jinsi zao zinatambulika. Anasema, inapolazimu kutofautisha majina kijinsi, *lokile* hutumika kwa dume na *naberu* kwa jike. Majina haya huwekwa mwishoni mwa jina ili kufafanua mnyama anayerejelewa ni wa jinsi ipi. Jinsi hutofautishwa kwa viambishi awali *lo-* (dume), *na-* (jike). Kwa upande mwingine, *ni-* hutambulisha mnyama ambaye amehasiwa. Wanyama wa hatua ya pili ni wale ambao wamepevuka na wanaweza kuzaa. Dume la hatua hii huweza kupanda jike na kusababisha mimba. Jike wa hatua hii huweza kupandwa, kubeba mimba, kuzaa, kunyonyesha na kukamuliwa. Dume la hatua hii hujulikana kwa jina la *la* (*lo-a)-ngitou* = *langitou* (mwenye korodani). Huyu ni yule ambaye bado hajahasiwa; ambaye anatarajiwa kuhasiwa huitwa *iwanitai*. Wanyama dume wa hatua ya tatu ni *akiduwar*. Wanyama jike wa hatua hii pia, kama wale wa hatua ya pili, wana uwezo wa kupata mimba. Wanyama walio na mimba wamegawanyika katika makundi matatu. Mosi ni *akikap*. Huyu ni mnyama mwenye mimba ambaye maziwa na chuchu bado havijakua. Ikiwa kiumbe kitazaliwa katika hatua hii, kitakuwa hakina nywele kabisa na hakitaweza kuishi. Pili ni *akiwochun*. Huyu ni mnyama mwenye mimba ambaye tumbo limekua. Hata asubuhi kabla ya kwenda machungani tumbo lake huwa limejaa kana kwamba ameshiba. Kiumbe kilichopo tumboni kikitoka katika hatua hii, kitakuwa na nywele kichwani na kwenye ncha za vidole vya miguu na mkiani, lakini hakiwezi kuishi. Tatu ni *akitaalakin*. Tumbo la mnyama huyu ni kubwa sana. Ameanza kutoa maziwa. Kiumbe wa tumboni akizaliwa katika hatua hii, huweza kuishi.

Kuhusu kigezo cha rangi, Ohta (1987) anasema kuwa kuna rangi mbalimbali za ngozi. Rangi hizo ni *-aakwan* (nyeupe), *-kiryoon* (nyeusi), *-aaryangan* (nyekundu), *-nyang* (njano au machungwa), *-ngori* (kijivu au kahawia), *-kipurat* au *-bok* (nyekundu na zambarau mpauko). Rangi hizo ndizo zinazotumiwa katika kutoa majina. Hata hivyo, baadhi ya ng'ombe huwa na rangi zaidi ya moja; kwa hiyo, ng'ombe hao hupewa majina kwendana na rangi zilizopo kwenye ngozi. Mathalani, *-meri* hutaja ng'ombe mweupe mwenye vidoa vyeusi (*-kiryoon*), ng'ombe mwenye rangi za bluu na kijani ataitwa *(-pus*), na zambarau (*-mugi*) na *-kori* hutaja ng'ombe wa rangi nyekundu *(-aryangan*), njano *(-nyang*), kijivu (*-ngori*) na nyekundu zambarau mpauko (*kipurat* au *-bok*).

Kigezo cha tatu, kama tulivyoona hapo juu ni umbo la pembe. Ohta (1987) anatoa mifano kadhaa ya majina ya wanyama yanayotokana na maumbo ya pembe. Mifano hiyo ni jina *-ita* ambalo hupewa ng'ombe wenye pembe kali zilizochongoka, -

*koda* kwa ng'ombe wenye pembe zinazoweza kubeba vitu, na *-dyepa* hupewa ng'ombe wenye pembe zisizolingana.

Kigezo cha nne ni umbo la sikio. Ohta (1987) anasema kuwa majina ya wanyama katika jamii ya Turkana hutolewa kwa kuangalia umbo la sikio yaani jinsi sikio lilivyokatwa au kurembwa. Mathalani, jina *-mulele* hupewa mnyama mwenye masikio mafupi yasiyozidi sentimeta 4; *-mudan* huitwa mnyama mwenye masikio yenye urefu wa sentimeta 4 hadi 8 na *itaangaki* ni mnyama mwenye masikio yenye urefu wa sentimeta zaidi ya 8.

Uchambuzi huu wa Ohta ni wa muhimu katika makala hii kwa sababu unaelekeza kutumia vigezo mbalimbali katika kubainisha majina ya wanyama. Hata hivyo, utafiti wake umebainisha majina ya jumla ya wanyama, na si majina mahususi. Utafiti uliozaa makala hii umeangalia utoaji wa majina ya mifugo kwa kila mfugo teule.

Imai (1982a) anabainisha majina ya kondoo, mbuzi, ngamia na ng'ombe kwa kutumia kigezo cha hali ya mnyama husika katika jamii ya Gabra[2]. Kwa mujibu wa Imai, kondoo na mbuzi wanapitia hali tano ambazo ni uchanga, upevukaji, uzazi, uhasiwaji, na udume. Ngamia na ngombe wanapitia hali nne ambazo ni uchanga, uzazi, uhasiwaji, na udume. Kila hatua huwa na jina lake kama mifano ifuatayo inavyoonesha:

| | **Kondoo** | **Mbuzi** |
|---|---|---|
| **Jina la jumla** | *olichi* | *lales* |
| **Dume** | *olemo korma* | *korbeji korma* |
| **Dume hasiwa** | *elemiji* | *korbeji* |
| **Jike aliyezaa** | *olichi* | *lales* |
| **Jike asiyezaa** | *kar sole* | *ilmele* |
| **Dume lisopevuka** | *elemiye* | *korbeji* |
| **Changa** | *mole ola au emola* | *mole lalesa au emole* |

| | **Ngamia** | **Ng'ombe** |
|---|---|---|
| **Jina la jumla** | *garr* | *ion* |
| **Dume** | *kingele* | *jibicha* |
| **Dume hasiwa** | *rotcho* | *sanga* |
| **Jike aliyezaa** | *orge* | *rada* |
| **Jike asiyezaa** | *goloms* | *goloms* |
| **Jike anayezaa** | *arra* | *sah* |
| **Dume changa** | *gurbo* | *yabi* |
| **Jike changa** | | *yabi* |

[2] Ni jamii ya kuhamahama ambayo inapatikana katika Jangwa la Chalbi na Ziwa Turkana na Marsabit, Kaskazini mwa Kenya na katika baadhi ya maeneo ya Ethiopia (Imai, 1982b).

Utafiti wa Imai una tija kubwa katika kuandika makala hii kwa sababu unaelekeza kubainisha majina ya wanyama kwa kuangalia hatua za ukuaji za wanyama husika.

Pia, Imai (1982b) alitafiti kuhusu utoaji wa majina ya mbuzi katika jamii ya Gabra. Alibainisha kuwa jamii ya Gabra hutoa majina ya mbuzi kwa kuzingatia jina la kikeni, pengine ni kile ambacho Chiwanga na Mkiramweni (2019) wanakiita matronimia (majina ya kutoka upande wa kike), yaani, ng'ombe jike huitwa kwa jina la ukoo wa upande wa mama (mfumo jike). Kwa hiyo, kila mbuzi huitwa kwa jina la mama yake. Jina la kwanza la mbuzi ni la ukoo (kikeni) na jina la pili linatokana na mwonekano wa mbuzi kama rangi na pembe. Rangi zinazotumika katika Gabra ni kama vile *adi* (nyeupe), *dimtu* (kahawia), *ble* (kijivu), na *grati* (nyeusi). Kwa hiyo, mbuzi akiitwa *adio moyeti*, *adio* linakuwa la ukoo (ukoo mweupe) na *moyeti* ni hali ya kutokuwa na pembe (jina la mwonekano). Imai anaeleza zaidi kuwa jina la pili hudondoshwa wakati mbuzi anaitwa kukamuliwa.

Maelezo ya Imai yametusaidia kufahamu kuwa mbuzi wanaitwa kwa namna mbalimbali kama kutumia vigezo vya ukoo (hasa wa kikeni) na mwonekano wa mnyama kama rangi na pembe. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa mifugo huitwa majina kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile ukoo, rangi za ngozi na pembe.

Deikumah, Konadu na Kwafo (2015) walifanya utafiti kuhusu utoaji wa majina ya ndege katika jamii ya Akan huko Ghana. Walibaini kuwa kuna vigezo vikuu vitano vya kuita ndege majina. Vigezo hivyo ni rangi, urukaji, tabia, ulaji, na makazi. Kwa kutumia kigezo cha rangi, kwa mfano, malimbe (*malimbes*) anaitwa *akyem polis* kwa sababu ni ndege mwenye rangi nyekundu na nyeusi. Neno *polis* maana yake ni polisi (askari) na linatokana na sare ya zamani ya askari polisi wa Ghana ambao walikuwa wakivaa kofia nyekundu pia. Kwa kutumia kigezo cha urukaji, pondagundi (*Goliath heron*) anaitwa *sohari* kutokana na miguu yake mirefu kama ya twiga inayomwezesha kwenda haraka. Kwa kutumia kigezo cha tabia, mathalani, kinega (*bee-eater*) anaitwa *bro-nya-noma*. *Noma* maana yake ni ndege. *Bronya* kwa lugha ya Akan ni Krismasi. Ndege hawa wanaitwa hivyo kwa sababu huonekana Kusini mwa Ghana kipindi cha ukame. Kwa kigezo cha ulaji, mbuawa (*prey*) anaitwa *akroma* kutokana na kuwinda na kula vetebrata wengine wadogo. Kwa kigezo cha makazi, korobindo kichwa-kijivu (*Northern grey-headed sparrow*) anaitwa *bola-noma* kwa sababu anapenda kuishi jalalani. Watafiti hawa wanasema kuwa ndege mmoja pia anaweza kupewa majina tofauti kulingana na vigezo tofauti. Ndege aitwaye kunguru (*the copied crow* au *corvus albus*), kwa mfano, ana majina matatu tofauti kutokana na vigezo vitatu tofauti pia ambavyo ni tabia, rangi na sauti/mwito. Majina hayo ni *akonkrain* (mla mizoga); *adene* (ndege mweusi); na *kwaakwaadabi* linalotokana na sauti kali ya ndege huyo (*kwaar - kwaar*).

Pamoja na wataalamu mbalimbali kutafiti suala la utoaji wa majina ya wanyama na ndege, ikiwamo mifugo katika jamii mbalimbali, bado hakuna utafiti uliozamia vigezo vinavyotumika kutoa majina ya mifugo katika jamii ya Gịrịmi, hususani Gịirwana. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na haja ya kutafiti zaidi suala la utoaji wa majina ya mifugo kwa jamii hiyo ili kubaini vigezo vinavyotumiwa pamoja na

mofolojia na semantiki ya majina hayo. Hii ni kwa sababu jamii zinatofautiana na, kwa hiyo, hatuwezi kuhitimisha mjadala wa utoaji wa majina ya mifugo kwa kutumia vigezo vya jamii zingine. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza vigezo vya utoaji wa majina katika jamii ya Gɪrɪ̣mi, hususani Gɪ̣irwana ili kuongeza maarifa kuhusu utoaji wa majina, hususani ya mifugo katika jamii hiyo.

## 4.0 Utoaji wa Majina ya Mifugo katika Gɪrɪ̣mi

Mifugo hujumuisha wanyama, ndege au wadudu wanaofugwa na binadamu (BAKITA, 2017). Arɪ̣mi hufuga wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda, mbwa na paka. Vilevile, hufuga kuku kwa wingi. Katika makala hii, mifugo itakayojadiliwa ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda na kuku kwa sababu ndiyo inayofugwa zaidi kuliko mingine katika jamii hiyo. Kama tulivyokwishaona katika kipengele kilichotangulia, kila jamii ina vigezo vyake vya utoaji wa majina kwa vitu vyake mbalimbali. Utafiti umebaini kwamba katika Gɪrɪ̣mi, vigezo vikuu vya kutoa majina kwa wanyama wafugwao ni vinne ambavyo ni ujinsi, rangi, umri na dosari.

## 4.1 Utoaji Majina ya Ng'ombe

Ng'ombe ni mnyama wa jamii ya nyati anayefugwa kwa ajili ya kupata nyama, maziwa au nguvu kazi (BAKITA, 2017). Kwa Gɪrɪ̣mi, jina la mnyama huyu linafanana na la Kiswahili, yaani *ng'ombe*. Kwa Arɪ̣mi, kwa mujibu wa utafiti, mnyama huyu ni mali ya thamani kubwa kuliko mali nyingine yoyote. Kipimo cha utajiri wa Mʊ̣rɪ̣mi ni idadi ya ng'ombe anaomiliki. Ng'ombe dume hutumika kulima kwa kutumia plau, na kukokota mikokoteni ya kubeba vitu kama vile mazao, miti na maji. Ng'ombe jike hukamuliwa, ambapo huwapatia Arɪ̣mi maziwa, jibini, siagi na samli. Pamoja na faida hizo, ng'ombe pia hutolewa kama mahari. Gharama za mahari hutolewa kwa hesabu ya ng'ombe ambao ni watano; majike wanne na dume mmoja. Majike wanakuwa wengi kwa sababu wanazaa na kuongeza utajiri wa ng'ombe (kwa anayepewa mahari) kwa haraka. Ikiwa unataka kuoa na huna ng'ombe, na unataka kutoa pesa, utatoa pesa inayolingana na bei ya ng'ombe ya wakati huo. Kwa Arɪ̣mi, samli ya ng'ombe hutumika kama mafuta ya baraka, ambapo watu hupakwa wanapofanya matambiko. Ng'ombe hupakwa samli wanapotolewa kama mahari ili wasikataliwe upande wa mwanamke anayeolewa na mke anayeolewa awe mwema. Jibini, siagi na samli pia hutumika kama chakula cha heshima kwa wageni. Kwa hiyo, ng'ombe ni mnyama mwenye thamani na anayeheshimika sana katika jamii ya Gɪrɪ̣mi. Kutokana na thamani ya ng'ombe kwa Mʊ̣rɪ̣mi, mtu asiye na ng'ombe hulazimika kuazima ng'ombe na kufuga, kitendo kinachoitwa *uvihwa ng'ombe*. Mwazimwaji hukaa na ng'ombe huyo na kufaidi mazao yote yatokanayo na ng'ombe huyo, ikiwamo kufanya kazi za shambani, isipokuwa umiliki unabaki kuwa wa mwenye ng'ombe. Ng'ombe wa kuazima akichinjwa na kuuzwa, fedha huwa ni za mmiliki. Utafiti umebaini kwamba utoaji wa majina ya ng'ombe kwa Arɪ̣mi huzingatia vigezo vikuu vinne ambavyo ni rangi, ujinsi, umri na dosari kama inavyojadiliwa katika vipengele vinavyofuata.

### 4.1.1 Kigezo cha Rangi na Ujinsi

Rangi (kwa Gɪ̣rɪ̣mi *ikerụ*) ndicho kigezo kikuu cha utoaji wa majina ya ng'ombe. Rangi ni kitu kinachotambulika kwa macho hata kwa mtu ambaye yupo mbali, ndio maana kinatumika kama kigezo kikuu cha utoaji wa majina kwa mifugo. Kigezo hiki hutumika pamoja na kigezo cha ujinsi, ambapo, kwa kiasi kikubwa, majina ya ng'ombe dume hutokana na majina ya ng'ombe jike. Kwa mujibu wa Msigwa (2018), ujinsi ni neno linalotofautisha kati ya a-kiume na a-kike. Msigwa anadai kuwa lugha zimegawanyika kijinsi katika makundi matatu: lugha zenye jinsi 'me', lugha zenye jinsi 'ke' na lugha zisojinsi. Anasisitiza kuwa mgawanyo huu hauwahusu watu peke yao, bali unajumuisha pia viumbe wengine kama vile wanyama na ndege, hali inayoonekana katika utoaji wa majina ya mifugo katika jamii ya Gɪirɪ̣mi pia isipokuwa usojinsi. Jedwali Na. 1 linatoa kwa muhtasari mifano ya majina ya ng'ombe yatumiwayo na Arɪ̣mi:

**Jedwali Na. 1: Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Rangi na Ujinsi**

| Na. | Jike | Dume | Rangi |
|---|---|---|---|
| 1. | *area* | *gídάarea* | hudhurungi/kahawia |
| 2. | *busɪ̣ni* | *gíbusɪ̣ni/ gídάmpondo* | kijivu iliyoiva |
| 3. | *bwasi* | *gídάbwasi* | nyeusi na baka kubwa jeupe ubavuni |
| 4. | *doghwani/ toghwani* | *gídoghwani/gítoghwani* | nyekundu |
| 5. | *ghofou* | *gídάghofou* | kijivu |
| 6. | *ghula* | *gídάghula* | nyeusi na madoa madogo mwilini |
| 7. | *lɪ̣ghɪ̣ni* | *gílɪ̣ghɪ̣ni* | nyeusi mwilini, weupe tumboni, shingoni na kifuani |
| 8. | *mara* | *gídάmaa* | nyeusi na nyeupe kichwani |
| 9. | *muryi* | *gídάmwi* | ugoro |
| 10. | *nyisi* | *gínyisi* | kijivu nyeupe |
| 11. | *sɪ̣ụli* | *gísɪ̣uli* | nyeupe pee |
| 12. | *samu* | *gísamu* | chuichui |
| 13. | *tɪ̣ti* | *gítụ* | nyeusi tii |
| 14. | *Ụmu* | *Gídumu* | Nyekundu na nyeusi |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Katika j

Katika Jedwali hili Na. 1, tunaona majina mengi ya ng'ombe dume yametokana na majina ya ng'ombe jike. Utafiti umebaini kuwa majina ya ng'ombe jike, kwa hiyo, yametumika kama mashina. Yamepachikwa viambishi awali kuunda majina ya ng'ombe dume. Viambishi vinavyopachikwa ni ***gí-***, ***gídά-*** kutegemeana na urahisi wa utamkaji wa neno. Ifahamike hapa kuwa viambishi vinavyoumba majina ya ng'ombe dume, hutamkwa kwa toni ya juu.

Kwa hiyo, utafiti pia umebaini kuwa mofolojia ya shina inatambulisha kwamba ng'ombe anayerejelewa ni jike na uambikaji wa viambishi ***gí-***, na ***gídά-*** hutambulisha kwamba anayerejelewa ni dume. Katika Jedwali Na. 1, tunaona majina ya ng'ombe jike yaliyoambikwa kiambishi ***gí-*** ni *doghwani*/*toghwani* (*gídoghwani*/*gítoghwani*), *busɪ̣ni*

(*gíbusịni*), *lịghịni* (*gílịghịni*), *nyisi* (*gínyisi*), *sịụli* (*gísịuli*), *samu* (*gísamu*) na *tịti* (*gítụ*). Majina ya ng'ombe yaliyoambikwa kiambishi ***gídá-*** ni *area* (*gídáarea*), *bwasi* (*gídábwasi*), *ghula* (*gídághula*), *mara* (*gídámaa)*, *muryi* (*gídámwi*) na *ụmu* (*gídumu*). Uambikaji huu unategemeana na urahisi wa kutamka jina la ng'ombe. Hata hivyo, wakati mwingine, mofolojia ya shina la ng'ombe dume inaweza kurekebishwa kwa sababu ya usahilishaji wa neno kimatamshi. Tuchukue mfano kutoka ng'ombe jike *mara*, jina la ng'ombe dume limekuwa *gídámaa*, ambapo sauti /**r**/ imedondoshwa. Jina la ng'ombe jike *tịtị* limebadilika na kuwa *gítụ*. Katika jina hili, mabadiliko makuu matatu yametokea. Mosi, silabi moja *ti* ya shina imedondoshwa. Pili, irabu mwisho *-ị* imedondoshwa, na tatu, irabu -u̱ imepachikwa mwishoni.

Katika uambikaji wa viambishi mwanzo katika mashina ya ng'ombe jike ili kupata jina la ng'ombe dume, mabadiliko ya kimofofonolojia pia huweza kutokea. Katika uambikaji wa majina, *ụmu* (*gídumu*), mathalani, irabu *-a* katika (*gídá*) imedondoshwa kwa sababu ya kufuatana na irabu *-ụ* iliyopo mwanzoni mwa shina la jina *ụmu*. Vilevile, katika jina la ng'ombe jike *muryi* mabadiliko yametokea. Kwanza, sauti -**ry-** zimedondoshwa. Sauti *-u-* ambayo imefuatana na irabu *-i* (*mui*) imeyeyushwa na kuwa *-w-*. Kwa hiyo, jina la ng'ombe dume limekuwa *gídámwi*.

### 4.1.2 Kigezo cha Dosari

Utafiti kuhusu utoaji wa majina kwa mifugo katika Gịirịmi umeonesha kuwa ng'ombe wenye dosari pia hupewa majina tofauti na ng'ombe wengine pamoja na kuwa na sifa zingine za kufanana na ng'ombe hao. Jedwali Na. 2 linaonesha majina hayo ya ng'ombe wenye dosari.

**Jedwali Na. 2: Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Ulemavu**

| Na. | Jina | Aina ya Ulemavu |
|---|---|---|
| 1. | *gíbúda* | ana korodani moja |
| 2. | *gínáwíída* | amezaliwa bila korodani |
| 3. | *gítụmpí* | ana mkia mfupi |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Katika Jedwali Na. 2, tunaona majina ya ng'ombe kwa kigezo cha ulemavu. Majina 1 na 2 *gíbúda* (ng'ombe mwenye korodani moja) na *gínáwíída* (ng'ombe ambaye amezaliwa bila korodoni) yanawahusu ng'ombe dume kwa sababu ndio wanaopaswa kuwa na korodani. Jina namba 3 *gítụmpí* linawahusu ng'ombe wa jinsi zote kwa sababu ng'ombe yeyote anaweza kuwa na mkia mfupi. Kwa hiyo, kiambishi *gí*, kwa mujibu wa utafiti, licha ya kuonesha jinsi me, kinaonesha hali ya ulemavu wa ng'ombe pia.

### 4.1.3 Kigezo cha Umri

Ni kawaida majina ya binadamu kubadilika kulingana na umri na mazingira. Mtu akiwa bado hajapata mtoto, mathalani, katika jamii ya Waswahili, huweza kutumia jina

aliloitwa na wazazi wake. Akipata mtoto, huweza kuitwa jina linalotokana na mwanaye wa kwanza kama vile Mama Yundu au Baba Yundu, yaani Yundu akiwa mtoto wa kwanza. Mbali na mabadiliko hayo ya majina kwa binadamu, utafiti umeonesha kuwa Arịmi pia hutoa majina ya ng'ombe kwa kuzingatia umri (hatua za ukuaji). Tuangalie Jedwali Na. 3 hapo chini:

**Jedwali Na. 3: Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Umri na Ujinsi**

| Na. | Umri | Dume | Jike |
|---|---|---|---|
| 1. | mdogo | *mwang'ombe/ganang'ombe/ganombe* | *mwang'ombe/ganang'ombe/ganombe* |
| 2. | kati | *mụjikụ* | *mụdama* |
| 3. | mkubwa | *njaghamba/jaghamba* | *ndama* |
| 4. | mzee | *njaghamba/jaghamba* | *mboghoma a ng'ombe* |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Utafiti umebaini zaidi kuwa ng'ombe akiwa mdogo, bila kujali jinsi, huitwa *mwang'ombe/ganang'ombe/ganombe*. Majina haya hutumika kwa ng'ombe ambaye ndio kwanza amezaliwa na aliye katika umri wa kunyonya. Baada ya hapo, majina huanza kugawanyika kutokana na jinsi. Hoja hii inafanana na ya Ohta (1987) anayesema kuwa katika hatua ya kwanza ya ukuaji, wanyama hawatofautishwi majina kijinsi hata kama jinsi zinafahamika isipokuwa inapolazimu kufanya hivyo. Kwa Arịmi, katika umri wa kati, ng'ombe dume hujulikana kwa jina la *mụjikụ*. *-jiku* ni nomino ya jumla ya ng'ombe dume ijapokuwa *njiku* hutumika kwa ng'ombe mbaye amehasiwa pia. Huyu ni ng'ombe wa rika la kati ambaye ametoka katika umri wa kunyonya, lakini bado hajaanza kufanya kazi kama vile kulima. Ng'ombe jike wa rika hili huitwa *mụdama*. Ng'ombe wa rika hili hawajafikia umri wa kuzaa. *Mụjikụ* na *mụdama* ndio ng'ombe wanaotumika kulipa mahari. Ng'ombe dume aliyepevuka hujulikana kwa jina la *njaghamba/jaghamba*. *Njaghamba* ni ng'ombe ambaye hajahasiwa. Ng'ombe huyu hutumika kama mtamba, yaani dume linalozalisha. Hufanya shughuli mbalimbali, hasa za shambani. Kwa upande mwingine, ng'ombe jike wa rika hili hujulikana kama *ndama*. Ng'ombe huyu huweza kubeba mimba na kuzaa. Kwa hiyo, huweza kukamuliwa na kumpatia mfugaji maziwa na mazao mengine kama jibini, siagi na samli. Ng'ombe jike mzee huitwa *mboghoma a ng'ombe*. *Mboghoma* ni neno linalotumika kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo hata kuku. Kwa hiyo, neno hili hufafanuliwa kwa kulihusianisha na mfugo husika kama tutakavyoona katika vipengele vitakavyofuata.

### 4.2 Utoaji Majina ya Mbuzi

Mbuzi ni mnyama wa kufugwa anayefanana na swala, mwenye pembe za ncha zinazoelekea nyuma (BAKITA, 2017). Mnyama huyu hufugwa na Arịmi pia. Jina lake la Gịrịmi ni *mbụri*. Utafiti umeonesha kuwa mbuzi hana thamani kubwa sana kama ng'ombe ila ana umuhimu pia. Mbuzi hutumika kama kitoweo, hasa kunapokuwa na mikusanyiko ya watu katika sherehe kama za jando, na shughuli kama za kusaidiana

kulima. Mbuzi pia hutumika kulipa mahari, ambapo idadi ya mbuzi huthaminishwa na ng'ombe. Vilevile, mbuzi ni mnyama anayefugwa kibiashara kwa ajili ya mahitaji madogomadogo na ya mara kwa mara. Kwa mujibu wa utafiti, mbuzi huitwa majina kwa kutumia vigezo vikuu viwili. Navyo ni ujinsi na umri kwa pamoja kama inavyowasilishwa katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Majina ya Mbuzi kwa Kigezo cha Umri na Ujinsi**

| Na. | Umri | Dume | Jike |
|---|---|---|---|
| 1. | mdogo | *gagwata/mwangwata/ganambụri/mwambụri* | *mwandoghoha wa mbụri, gadoghoha ga mbụri, ganambụri/mwambụri* |
| 2. | kati | *mụgwata* | *mụdoghoha wa mbụri* |
| 3. | mkubwa | *ngwata* | *ndoghoha a mburi* |
| 4. | mzee | *ngwata* | *mboghoma a mbụri* |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Katika Jedwali Na. 4, tunaona majina ya mbuzi yanatofautiana kulingana na hatua za ukuaji. Mbuzi dume mchanga ana visawe vinne: *gagwata*, *mwangwata*, *ganambụri*, na *mwambụri*, na mbuzi jike ana visawe vinne: *mwandoghoha wa mbụri*, *gadoghoha ga mbụri*, *ganambụri*, na *mwambụri*. Mbuzi wadogo wa jinsi zote wanatumia visawe viwili ambavyo ni *ganambụri* na *mwambụri*. Viambishi *ga*-, *gana*- na *mwa*- ni vya udogoshaji. *Ga*- na *gana*- vinaonesha vimbuzi ni vidogo kabisa na *mwa* kinaonesha vimbuzi ni vikubwavikubwa. Vilevile, mbuzi dume wa hatua hii huitwa *gagwata*/*mwangwata*. *-gwata* ni shina linaloonesha mbuzi dume na hutumika kwa mbuzi dume tu. *-doghoha* ni shina la nomino linaloonesha mfugo (mbuzi/kondoo/kuku) wa kike. Mbuzi dume wa rika la kati anaitwa *mụgwata* na jike huitwa *mụdoghoha wa mbụri*. *Mụ*- ni kiambishi kinachoonesha kuanza kupevuka (ukati). Kwa mujibu wa utafiti, mbuzi wa hatua hii ameacha kunyonya ila hawezi kuzaa. Mbuzi dume mkubwa huitwa *ngwata* na jike ni *ndoghoha a mburi*. Kiambishi *n*- kinaonesha upevu wa mbuzi husika. Mbuzi hawa ni wakubwa na wanaweza kuzaa. *Ngwata* anakuwa hajahasiwa. Mbuzi aliyehasiwa huitwa *mpahi* (dume). *Mpahi* ni jina linalotumika kwa mbuzi tu. Kwa hiyo, kwa sababu mbuzi huyu amehasiwa, hazururi ovyo kutafuta majike. Kwa hiyo, ni mtulivu. Anakuwa na umbo kubwa na kilo nyingi. Mbuzi huyu hufaa kwa biashara kwa sababu huweza kuuzwa kwa bei kubwa. Mbuzi jike mzee huitwa *mboghoma a mburi* (jike). *Mboghoma* ni neno linalotumika kwa ng'ombe, mbuzi, kondoo hata kuku jike kama tulivyoona katika sehemu ya utoaji wa majina ya ng'ombe.

### 4.3 Utoaji Majina ya Kondoo

Kondoo ni mnyama wa kufugwa anayefanana na mbuzi mwenye manyoya mengi kuliko mbuzi (BAKITA, 2017). Katika Gɪrɪmi, mnyama huyu huitwa *nkhoo*. Kulingana na utafiti uliofanyika, kondoo, kama ilivyo mbuzi, hutumiwa kama kitoweo. Kondoo

pia ni mnyama wa tambiko, yaani nyama yake hunenewa maneno ya kitambiko na kuliwa tambikoni. Kama ilivyo kwa mbuzi, kondoo pia hutumika kulipa mahari, ambapo idadi ya kondoo huthaminishwa na gharama ya ng'ombe. Kondoo huitwa majina kwa kutumia vigezo vikuu viwili pia. Navyo ni ujinsi na umri kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5 lifuatalo:

**Jedwali Na. 5: Majina ya Kondoo kwa Kigezo cha Umri na Ujinsi**

| Na. | Umri | Dume | Jike |
|---|---|---|---|
| 1. | mdogo | *ganankhoo/mwankhoo/ganankhambaku/ gakhambaku/mwankhambaku* | *ganankhoo/mwankhoo/gadoghoha ga nkhoo/ mwandoghoha wa nkhoo* |
| 2. | kati | *mʉkhambaku* | *mʉdoghoha wa nkhoo* |
| 3. | mkubwa | *nkhambakʉ* | *ndoghoha a nkhoo* |
| 4. | mkubwa/mzee | *nkhambakʉ* | *mboghoma a nkhoo* |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Kutoka katika Jedwali Na. 5, tunaona majina ya kondoo katika Gɪrɪmi yanagawanywa katika hatua nne za ukuaji. Utafiti umeonesha kuwa kondoo dume na jike wakiwa wadogo wanachangia majina mawili. Majina hayo ni *ganankhoo* na *mwankhoo*. Kondoo dume mdogo anaitwa *ganankhambaku*/*gakhambaku*/ *mwankhambaku* na kondoo jike mdogo ni *gadoghoha ga nkhoo*/*mwandoghoha wa nkhoo*. Kama tulivyokwishaona, viambishi *ga*-(*na*-)/*mwa*- vinaonesha udogo wa mfugo. -*nkhoo* ni shina linalotaja nomino kondoo. -*khambaku* ni shina la jina la kondoo dume. Jina hili hutumika kwa kondoo dume tu na si vinginevyo. Kondoo dume wa rika la kati ni *mʉkhambaku* na jike ni *mʉdoghoha wa nkhoo*. Kama tulivyokwishaona, -*doghoha* ni nomino inayoonesha mfugo wa kike. Kwa hiyo, *mʉdoghoha wa nkhoo* maana yake ni kondoo jike, yaani maneno *wa nkhoo* (wa kondoo) ni ufafanuzi wa mfugo jike unaorejelewa ambao ni kondoo. *Mʉ*- ni kiambishi kinachoonesha kuanza kupevuka. Kwa ujumla, kondoo wa hatua hii ni wale waliotoka katika umri wa kunyonya, lakini bado hawajapevuka kuweza kuzaa. Kondoo wakubwa ni *nkhambakʉ* (dume) na *ndoghoha a nkhoo* (jike). *Nkhambakʉ* wa hatua hii anakuwa hajahasiwa. Tumekwishasema wakati tunajadili kuhusu utoaji majina ya mbuzi kuwa kiambishi *n*- kinaonesha kuwa mfugo umepevuka. Kwa hiyo, kondoo wa umri huu wana uwezo wa kuzaa. Katika umri wa uzee, kondoo dume anaendelea kuwa na jina lilelile la hatua ya ukubwa. Kondoo huyu anaweza kuwa amehasiwa au hajahasiwa. Kama ilivyo kwa *mpahi*, *nkhambakʉ* aliyehasiwa, anakuwa na umbo kubwa; kwa hiyo, anafaa kwa biashara kwa sababu anaweza kuuzwa kwa bei kubwa. Jina la kondoo jike mzee ni *mboghoma a nkhoo*.

### 4.4 Utoaji Majina ya Punda

Punda ni mnyama wa kufugwa anayefanana na farasi mwenye rangi nyeupe au hudhurungi ambaye hutumika kubeba mizigo. Katika Gɪrɪmi, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, mnyama huyu huitwa *ndoghwe* na lakabu yake ni *mʉhɪngɪlɪ*. Nyama ya

punda hailiwi na watu wengi. Wengi wanaionea kichefuchefu. Hata hivyo, utafiti umeonesha kuwa nyama hiyo inatumika kama tiba ya majipu. Maziwa ya punda hayatumiki kama chakula cha kawaida isipokuwa hutumika kama tiba ya kifua na pumu, hasa kwa watoto wadogo. Punda ni mnyama anayetumika kubeba mizigo bila kujali kama ni dume au jike. Hubebeshwa mizigo mgongoni na huweza kutembea mwendo mrefu bila kuchoka. Punda pia hutumika kulimia kwa kutumia plau. Utafiti umeonesha kuwa tofauti na wanyama wengine, punda ana jina moja tu. Hakuna mgawanyo kwa kuzingatia jinsi wala kigezo kingine kwa sababu punda wote (dume na jike) hufanya kazi zinazofanana kwa usawa na, pengine, wana rangi mbili tu, nyeupe na hudhurungi. Hata hivyo, mtoto wa punda huitwa *ganandoghwe*/*mwandoghwe*.

**4.5 Utoaji wa Majina ya Kuku**

Kuku ni ndege mkubwa anayefugwa na anafanana na kware mkubwa (TUKI, 2013). Kwa Gịrịmi, ndege huyu huitwa *ηkụkụ*. Kwa Arịmi, kwa mujibu wa utafiti, nyama na mayai ya kuku ni vitoweo. Nyama ya kuku ni kitoweo cha heshima kubwa kwa wageni. Mgeni wa heshima huchinjiwa kuku, hata kupewa zawadi anapoondoka. Kuna desturi ya muda mrefu ya wapwa kupewa kuku wadogo wa kufuga na wajomba zao. Hata kama wajomba ni wengi, kila mjomba anawajibika kumpa mpwa wake kuku. Katika jamii hii, inaonekana kuwa ni haki ya kila mpwa kupewa kuku wa kufuga hata bila kuomba. Utafiti umeonesha kuwa kuku ni mfugo unaotumika katika tiba za kienyeji. Mgonjwa huagizwa kupeleka kuku wa rangi moja (mweusi, mweupe au mwekundu), ambapo kuku huyu huchinjwa kwa mganga na kupikwa supu iliyochanganywa na dawa. Baada ya supu kuiva, mgonjwa hupewa anywe. Amalizapo kunywa, huingiza unyoya wa kuku kwenye koromeo na kutapika ili ugonjwa umtoke. Zaidi, utafiti umebaini kuwa, kama ilivyo kwa mifugo mingine, kuku hupewa majina kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni ujinsi na umri kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 6 lifuatalo:

**Jedwali Na. 6: Majina ya Kuku kwa Kigezo cha Umri na Ujinsi**

| Na. | Umri | Dume | Jike |
|---|---|---|---|
| 1. | uchanga | *ganaηkụkụ/gaηkụkụ/mwaηkụkụ* | *ganaηkụkụ/gaηkụkụ/gakụkụ mwaηkụkụ* |
| 2. | udogo | *gananjololo/gajololo/mwanjololo/* | *Ganandoghoha ga ηkụkụ/gadoghoha ga ηkụkụ/mwandoghoha wa ηkụkụ* |
| 3. | ukati | *mụjololo* | *mụdoghoha wa ηkụkụ* |
| 4. | ukubwa | *njololo* | *Ndoghoha a ηkụkụ* |
| 5. | uzee | *njololo* | *mboghoma a ηkụkụ* |

**Chanzo:** Data za Utafiti (2020)

Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa kuku ana hatua tano za makuzi tangu anapotoka kwenye yai. Hatua hizo ni uchanga (ufaranga), udogo, ukati, ukubwa na uzee. Katika hatua ya kwanza, kuku hatambuliki jinsi yake. Kwa hiyo, kuku yeyote wa hatua hii huitwa g*anaηkụkụ*/*gaηkụkụ*/ *gakụkụ/mwaηkụkụ*. Kama kawaida *gana*-, *ga*- na *mwa*- ni viambishi vinavyoonesha udogo wa mfugo (katika kipengele hiki mfugo ni kuku). -

*kụkụ* ni shina linalobeba jina kuku. Utafiti umebaini kuwa katika hatua ya udogo, kuku anaanza kujulikana jinsi yake, hasa baada ya kuota mabawa. Kwa hiyo, majina ya kuku huanza kutengwa kwa kuzingatia jinsi ya kiume na ya kike katika hatua hii. Kuku dume wa ngazi hii hujulikana kama *gananjololo*/*gajololo*/*mwanjololo*. *-jololo* ni shina linalotaja kuku dume (jogoo) na hutumika kwa jogoo tu. Kuku jike wa hatua hii huitwa *ganandoghoha/gadoghoha/mwandoghoha*. Shina *-doghoha* limekwisha- elezewa katika sehemu zilizotangulia kuwa linahusu mfugo wa kike ndio maana linahusishwa na jina la mfugo husika kama tulivyoona katika utoaji wa majina ya mbuzi na kondoo. Katika ngazi ya tatu (ukati), kuku dume huitwa *mụjololo* na jike huitwa *mụdoghoha wa ηkụkụ*. Kuku wa rika hili wamepevuka, lakini hawawezi kuzaa. *Mụdoghoha,* kwa mujibu wa utafiti wetu, ndiye kuku anayefaa kugawiwa kwa wapwa kwa sababu amevuka katika hatari ya kushambuliwa na mwewe na vicheche; kwa hiyo, anaweza kufugika. Kuku wa hatua ya nne (ukubwa) ambao ni *njololo* na *ndoghoha a ηkụkụ* wamepevuka na wanaweza kuzaa. Kwa kawaida, *njololo* huwa mmoja tu nyumbani kwa sababu wakiwa wengi huweza kupigana na hata kuumizana kwa sababu ya majike. Kwa sababu hiyo, *njololo* huweza kufugwa mpaka kufikia hatua ya uzee akiwa na jina hilohilo. Utafiti unaonesha kuwa *ndoghoha a ηkụkụ*, aghalabu, ni jina linalotumika kwa kuku jike ambaye amepata watoto awamu moja tu. Baada ya hapo huitwa *mboghoma a ηkụkụ*, ambalo ni jina la uzee.

## 5.0 Hitimisho

Majina ni muhimu katika mawasiliano ya kila siku ya binadamu. Majina hutambulisha kirejelewa. Kwa hiyo, ni rahisi kuelewa kinachotajwa kwa kutumia jina lake mahususi. Makala hii, kutokana na umuhimu huo, imechambua majina ya mifugo katika Gịrịmi, hususani Gịirwana. Mifugo iliyojumuishwa katika utafiti uliozaa makala hii ni ng’ombe, mbuzi, kondoo, punda na kuku. Makala inaonesha kuwa vigezo vikuu vilivyotumika katika utoaji wa majina ya mifugo ni vinne. Vigezo hivyo ni umri, ujinsi, rangi na dosari. Vigezo hivyo huweza kutumika peke yake katika utoaji wa majina au vigezo viwili hutumika kwa pamoja. Ng’ombe huitwa kwa kutumia ujinsi na rangi kwa pamoja; kwa kutumia dosari (ulemavu); na umri pamoja na ujinsi. Mifugo mingine hutumia umri na ujinsi isipokuwa punda ambaye anatumia kigezo kimoja tu ambacho ni umri. Aidha, matokeo ya utafiti yameonesha, katika hatua ya kwanza ya kuzaliwa, mifugo mingi huwa na majina yanayofanana na majina huanza kugawanywa kwa kuzingatia ujinsi katika hatua ya pili. Makala hii inapendekeza uchunguzi zaidi wa utoaji wa majina ya mifugo kuendelea kufanyika ili kuimarisha mawasiliano katika jamii mbalimbali za wafugaji na kuyahifadhi majina hayo kwa ajili ya vizazi vijavyo.

## Marejeleo

BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Longhorn Publishers Limited.

Chiwanga, F. na Mkiramweni, N. (2019). “Ethno-ornithology and Onomastics in the Natta Community, Serengati District.” *Heliyon* 5: 1 - 6.

Deikumah, J., Konadu, V. na Kwafo, R. (2015). Bird Naming System by Akan People in Ghana

Imai, I. (1982a). "Subsitence Ecology of the Paatoral Gabra: A Preliminary Report . *African Study Monographs*," 2.

Imai, I. (1982b). "Small Stock Management and the Goat Naming System of the Patroral Gabra. *African Study Monographs*, *Supplementary Issue*," 1: 43 - 62.

Montagnes, I. (1991). *Editing and Publication.* Ottawa: International Development Research Center.

Msigwa, A. (2018). "Ujinsi wa Nomino za Mkopo katika Kiswahili". *JULACE*, 3(2): 23 - 31.

Ohta, I. (1987). "Livestock Individual Identification among the Turkana: The Animal Classification and Naming in the Pastoral Livestock Management." *African Study Monographs*, 8 (1): 1 - 69.

Okal, B. (2012). "Nafasi ya Tafsiri katika Taaluma ya Onamastiki: Uhakiki wa Mbinu zake katika Tafsiri ya Toponomastiki." *Kiswahili*, 75: 27 - 42.

Olson, H. (1964). *The Phonology and Morphology of Rɪmi.* Connecticut: Hartford Studies in Linguistics.

Resani, M. (2016). Maana katika Majina ya Wabena Nchini Tanzania. *Mulika*, 35: 98 - 113.

Stephano, R. (2019). "Gɪrɪmi Reduplication and Its Alternative Representation: The Case of Gɪirwana." *JAKIIKI*, Toleo Maalumu, 206 - 213.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, toleo la tatu. Dar es Salaam: TUKI.

Wilson, A. (2014). Tofauti za Kimsamiati katika Lahaja za Kinyaturu. Tasnifu ya Shahada ya Umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.